



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

WAKALA WA BARABARA ZA VIJJINI NA MIJINI-TANZANIA
(TARURA)

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development

S.L.P. 34314,
DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA UMMA

Dar es Salaam, Tanzania – (Machi 25, 2024)

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (**OR-TAMISEMI**) kupitia kitengo cha Uratibu wa Mradi wa Bonde la Msimbazi (Project Coordination Unit (PCU) kinachosimamiwa na Wakala ya Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), inautaarifu umma kuanza kwa zoezi la ubomoaji wa nyumba zilizofidiwa na Mraadi wa Uendelezaji wa Bonde la Msimbazi.

Kwa mujibu wa makubaliano ya utekelezaji wa zoezi hili, waathirika wa mradi ambao wameshahapeka malipo yao wanatakiwa kuhamisha mali zao na kupisha eneo la mradi ndani ya **wiki sita (6)** baada ya kupokea fedha hizo kwenye akaunti zao. Muda huo umeshakamilika kwa idadi kubwa ya waathirika ambapo mpaka kufikia tarehe **21 Machi 2024**, tayari waathirika **2,155** wamelipwa kiasi cha **shilingi 52,612,072,623.15** kati ya **2,329** waliopo kwenye daftari la kwanza la daftari wamekwishahapeka malipo yao.

Ofisi ya uratibu wa mradi, kwa kushirikiana na ofisi za wakurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni, inatarajia kuanza zoezi la ubomoaji wa nyumba zilizofidiwa kuanzia tarehe **12 Aprili 2024**. Hivyo wananchi wote ambao wamekwishalipwa fidia wanatakiwa kuondoka katika maeneo yao kabla ya tarehe hiyo.

Hata hivyo, awamu hii ya utekelezaji wa zoezi hili itawahuisha wale ambao wamefikisha **wiki sita (6)** zilizotolewa baada ya kupokea malipo ya fidia hadi kufikia tarehe **29 Februari 2024**.

Aidha, daftari la pili fidia la waathirika **446** ambao hawakufikiwa katika uthamini wa awali kwa sababu mbalimbali limeshakamilika na litawasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kusainiwa siku ya jumanne tarehe **26 Machi 2024** tayari kwa kulipwa fidia.

Wananchi ambao wanamaswali au wanahitaji maelezo zaidi kuhusu zoezi la ubomoaji wanaweza kuwasiliana na ofisi ya uratibu wa mradi wa Bonde la Msimbazi kupitia namba namba ya “**What's app**” **0738353854** kwa kutuma ujumbe au piga namba **0738353855** kupata majibu ya maswali yako yote kuhusu zoezi hili.

Imetolewa na:

Mhandisi: Kanyenye, H.N

Mratibu wa Miradi ya Ushirikiano na Benki ya Dunia
TARURA.

Ghorofa ya 4, LAPF Millennium Towers, Kijitonyama, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi. Simu: 255 (22)2700765/69
Nukushi: 255 (22) 2700768 Barua pepe: cities.project@tamisemi.go.tz, cities.project@yahoo.com Tovuti: www.tarura.go.tz

TARURA ni Wakala uliopo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ulioanzishwa chini ya Sheria za Uanzishwaji wa Wakala "Executive Agency Act, CAP 245"